

121

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA KUKODISHA GARI KWA AJILI YA KUSAFIRISHA VIFAA VYA UJENZI -  
SQUARE PIPES, KUTOKA DAR ES SALAAM KWENDA UTETE RUFIFI

KWA AJILI YA UJENZI WA CHUO CHA VETA RUFIFI

MKATABA NA: PA/024/2021/22/TRA/RUF/DVTC/04

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 25 mwezi 02 - 2022

### KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha PWANI, S.L.P. 30345, KIBAHA, PWANI ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

M/S PASCHAL & SONS TRANSPORT COMMISION AGENT wa S. L. P.70981 DAR ES SALAAM. (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni wa usafirishaji vifaa") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIJI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIJI;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya RUFIJI ambayo ujenzi wake unaendelea;

### HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

#### 1. GHARAMA ZA USAFIRISHAJI

Kwamba, kwa għarama ya Shilingi za Tanzania 1,600,000/= kwa kuasafirisha vifaa vya ujenzi kutoka Dar es Salaam mpaka eneo la ujezi Utete Rufiji kama inavyoonekana kwenye jedwari hapo chini kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu,kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama za usafirishaji vifaa vya ujenzi"

Gharama za kazi zitakazofanyika katika kila jengo ni kama ifuatavyo:

S/N	STAGE	BEI ILIYOKUBALIKA
1	GHARAMA ZITAKAZOTUMIKA KUSAFIRISHA VIFAA VYA UJENZI(SQUARE PIPES) KUTOKA DAR ES SALAAM KWENDA ENEO LA UJENZI UTETE RUFIFI.	1,600,000
	JUMLA	1,600,000

**2. MABADILIKO YA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI (TRANSPORTATION SUM ADJUSTMENT)**

Gharama za usafirishaji hazitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko yoyote yaliyofanywa na Mwajiri.

**3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Malipo yatafanyika baada ya kazi kukamilika yaani Mzigo kufika eneo la ujenzi ukiwa salama na kwa idadi na kiwango kilichotakiwa.

**4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

(a) Mzabuni wa usafirishaji atakabidhi mzigo kwa wahusika wakuu waliopo eneo la ujenzi na kusainisha hati za mapokezi na nyaraka zingine muhimu kuonesha uhalali wa mapokezi ya mzigo husika.

(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Mzabuni wa usafirishaji kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo pasipo kuathiri pande zote.

**5. WAJIBU WA MZABUNI WA USAFIRISHAJI**

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kusafirisha mzigo wa vifaa vya ujenzi kwa kadri alivyokubaliana katika mkataba sambamba na maelekezo ya Mwajiri.

(b) Kumjulisha Mwajiri kuhusu mapungufu au mkanganyiko wowote utakaobainika

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA  
PWANI (PWANI RVTSC)

Jina:

CLARA KIBODYA Saini:

Subeley P

Wadhifa:

AG PRINCIPAL

Tarehe:

25/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina:

LUKA C. MJKIN Saini:

Abd

Wadhifa:

MJKIN KAMASI  
YA LESTARI

Tarehe:

25/02/2022

IMESAINIWA NA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Jina:

PASCHAL RAINA

Mbele ya

Saini:

PP

Wadhifa:

DIRECTOR

Tarehe:

25/02/2022



Mbele ya (Shahidi)

Jina:

Julius Jonas

Saini:

W. J. Munyaga

Wadhifa:

SECRETARY

Tarehe:

25/02/2022